

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA TANO**

**08 APRILI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA TANO – TAREHE 08 APRILI, 2024**

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**52. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Mtandika hadi Nyanzwa - Kilolo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**53. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Madaraja kwenye Barabara za Misughaa hadi Kikio na Matongo hadi Mpetu - Singida.

**54. MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa Hospitali kongwe ya Magunga - Korogwe.

**55. MHESHIMIWA ABEID RAMADHANI IGHONDO (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kununua Jenereta Hospitali ya Ilongero na Vituo vya Afya Mgori, Makuro na Msange - Jimbo la Singida Kaskazini.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**56. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kwa nini Serikali haielimishi Wananchi kujiepusha na madhara yatokanayo na athari za Mabadiliko ya Tabianchi hadi maafa yatokee.

#### **WIZARA YA FEDHA:**

#### **57. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, upi mkakati wa Serikali wa kuweka huduma za Wakala wa Forodha katika Bandari ya Nyamisati.

#### **WIZARA YA AFYA:**

#### **58. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, upi mpango wa kurejesha TFDA kwani imeacha masuala ya chakula na inakinzana na utaratibu wa usimamizi wa chakula na dawa Duniani.

#### **WIZARA YA UJENZI:**

#### **59. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itazuia kupaki magari ya Serikali sehemu za starehe baada ya masaa ya kazi.

#### **WIZARA YA UCHUKUZI:**

##### **60. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Wananchi wa Nachingwea ambao mashamba yao yalitwaliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege watalipwa fidia.

#### **WIZARA YA MAJI:**

##### **61. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mkandarasi anaejenga mradi wa maji Kata ya Mabaranga - Kilindi atakamilisha kazi hiyo.

#### **WIZARA YA KILIMO:**

##### **62. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mradi wa *Building Better Tomorrow* katika Bonde la Mto Rufiji.

#### **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**63. MHESHIMIWA SALIM ALAUDIN HASHAM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatoa majibu juu ya umiliki wa Msitu wa Hewa ya Ukaa uliopo Kituti hadi Mgolo.

#### **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**64. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, kuna mpango gani wa kuyafanya mafunzo ya Mgambo kuwa sehemu ya mafunzo kwa Vijana wanaokosa nafasi ya Kujiunga na JKT.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA  
YA HABARI:**

**65. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE  
(NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga minara ya Mawasiliano  
katika Kata ya Litapunga – Nsimbo.

**III. UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE:**

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri  
Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
08 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**